

KISWAHILI

KIDATO CHA 3

JINA..... NAMBARI.....

INSHA Alama 20

1. Anza kwa: Mwanangu, dunia imebadilika pakubwa. Lakini chungu mabadiliko hayo yasikuzuzue.....

MATUMIZI YA LUGHA

1. Tofautisha sifa za vipasuo /p/ na /b/ (Al 2)

2. Ni sifa zipi zinazotumiwa kuchunguza jinsi konsonanti zinavyotamkwa? (al 3)

3. Tambua vielezi katika sentensi ifuatayo (al 2)
 - Hamali na Kibe wataenda Mombasa kesho kutwa.

4. Tunga sentensi mbili mbili kuonyesha maana tofauti za maneno uliyopewa. (al 4)
Mbuzi -

Mlango -

5. Akifisha sentensi ifuatayo (al 3)
 - Bwana baraka huenda mjini kila jumapili kutazama mchezo wa kuigiza wa vioja mahakamani.

6. Bainisha aina za maneno katika sentensi zifuatazo (al 4)

(i) Cheti cha pamoja kimepatikana

(ii) Lo! Fisi amepanda juu ya mti

7. Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo (al 2)

Zubeda alimwandikisha Ali barua

8. Tambua nyakati katika sentensi zifuatazo (al 2)

(i) Jana kulinyesha mvua kubwa

(ii) Mimi ninajibu maswali

9. Tumia kirejeshi 'amba ' badala ya 'o' rejeshi katika sentensi ifuatayo. (al 2)

Uwanja uliopandwa miti ni wa mjombangu

10. Akifisha sentensi ifuatayo ili iwe katika hali tatu tofauti. (al 3)

Rais amewasili

11. Eleza ritifaa imetumika vipi katika sentensi (al 2)

(i) Ngombe wa jirani amepotea

(ii) Nilimwonya `ngawa hakun`sikia

12. Kanusha sentensi ifuatayo; (al 2)

Sungura amekufa

13. Geuza sentensi zifuatazo ziwe katika kauli ya kutendea (al 2)

(i) Kasiva aliandika barua ya indeche

(ii) Msetu alikula chakula cha motto

14. Andika sentensi zifuatazo kwa udog (al 2)

(i) Mji huu una watu wengi

(ii) Meza yangu kubwa imevunjika

SEHEMU C: ISIMU JAMII

Long'i ni mia, pata na mia, pata na mia, hundred bob tu, kuona ni bure. Viatu ni za aina yote. Buda karibu ujionee. Niaje maze come tu..... Come tu, karibia ujionee. Hata za manzi ziko. Mali motomoto kutoka ng'ambo. Watu wote wabuy huku! Dungarees ni soo mbili.....za watoi na wasupa.

(a) Eleza muktadha wa mazungumzo haya. (al 2)

(b) Eleza sifa za lugha itumiwayo katika sajili hii kama zinavyojitokeza katika kifungu.